



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA



*Unapojibu tafadhali taja:*

Kumb.Na.MZA/KDC/S.10/40/79

27 Aprili, 2023

**Yah: MABADILIKO YA TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba alitangaza nafasi za kazi za Mtendaji wa Kijiji Daraja III nafasi 12, Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II nafasi 2 na Dereva Daraja la II nafasi 5 kupitia Tangazo lenye kumb.Na. MZA/KDC/S.10/40/78 la tarehe 20/04/2023 baada ya kupokea kibali cha ajira mpya kwa mwaka 2022/2023 chenye Kumb. Na. FA.97/228/01'TEMP'/06 cha tarehe 06 Aprili,2023 na Kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb.Na.FA.170/359/01"B"/72 cha tarehe 21/02/2023 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba amepokea maelekezo kutoka kwa Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa barua yenye Kumb Na. AB.161/259/01/D/12 ya tarehe 20 Aprili,2023 kuwa kwa mujibu wa Kanuni Namba ya 22(1-2) ya kanuni za Uendeshaji wa shughuli za Sekretarieti ya Ajira kama ilivyoboreshwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 580 la 2022 kuwa inaainisha kutumika kwa **kanzi data** ya waliofaulu usaili lakini hawakuweza kupangiwa vituo vya kazi pale inapotokea fursa ya Ajira.

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba ilitangaza nafasi 14 za Mtendaji wa Kijiji Daraja III na nafasi 4 za Dereva Daraja la II na kufanya usaili mwezi Julai, 2022 ambapo wasailiwa wengi walifaulu na kwa kuwa nafasi zilikuwa chache hawakupagiwa vituo vya kazi. Hivyo, wasailiwa hao waliofaulu na kukosa fursa ya kuajiriwa wataitwa kujaza nafasi 12 za Mtendaji wa Kijiji Daraja la III na nafasi 2 za Dereva Daraja la II zilizotangazwa kupitia Tangazo la nafasi za kazi lenye Kumb.Na. MZA/KDC/S.10/40/78 la tarehe 20/04/2023.

Kwa mantiki hiyo **ninasitisha maombi ya kazi ya nafasi 12 za Mtendaji wa Kijiji Daraja la III** kwa sababu zitajazwa na wasailiwa waliofaulu katika usaili uliofanyika tarehe 07 na 08 Julai, 2022 ambao taarifa zao zipo kwenye **kanzi data** ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba na wakakosa nafasi za kazi.

Kwa upande wa nafasi 5 za Dereva Daraja la II zitajazwa nafasi mbili (2) kwa kutumia **kanzi data** ya wasailiwa waliofaulu katika usaili wa nafasi za Dereva Daraja la II uliofanyika tarehe 05/07/2022 kwa sababu ni wasailiwa wawili tu waliofaulu na kukosa nafasi. Hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba kwa nafasi za Dereva Daraja la II zinabaki nafasi tatu (03) ambazo waombaji wataendelea kutuma maombi ya kazi.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba haikuwa na nafasi za kazi kwa Kada ya Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II katika Tangazo la Kazi lenye Kumb.Na.MZA/KDC/S.10/40/42 la tarehe 24/05/2022. Hivyo, nafasi mbili (2) za Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II zitaendelea kubaki kama ilivyo kwenye Tangazo la nafasi za kazi lenye Kumb.Na. MZA/KDC/S.10/40/78 la tarehe la tarehe 20/04/2023 na mwisho wa kutuma maombi ya kazi itakuwa tarehe 05/05/2023 kama ilivyokuwa kwenye Tangazo.

Ninaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba [www.kwimbadc.go.tz](http://www.kwimbadc.go.tz)

Tangazo hili limetolewa na;

**H**  
H.J.MSANGA  
MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA KWIMBA.

*MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KWIMBA*

---

Mtaa wa Kakora, S.L.P 88, Ngudu, SIMU:+255 (028) 2983121,Nukushi: +255 (028) 2983119  
Barua Pepe: [ded@kwimba\\_dc.go.tz](mailto:ded@kwimba_dc.go.tz) ,[dhro@kwimbadc.go.tz](mailto:dhro@kwimbadc.go.tz) , Tovuti: [www.kwimbadc.go.tz](http://www.kwimbadc.go.tz)

Uk. 2